**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2024**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

Mkuu wa Shule 0688 227150
Makamu Mkuu wa Shule. 0713 042844
Matron/Patron 0683 104790
Shule ya Sekondari Hombolo
S.L.P. 1719
Tarehe 01.06.2024

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….
…………………………………………….
S.L.P ……………………………………
…………………………………………….

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI HOMBOLO HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA MKOA WA DODOMA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024/ na atasoma tahasusi ya PCM/PCB

Shule ya Sekondari Hombolo ipo umbali wa Kilometa 45 Kaskazini/Mashariki mwa Jiji la Dodoma, njia kuu ya kuelekea mkoani Dar es salaam. Usafiri wa basi kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi yaendayo vijijini kilichopo katika soko maarufu la Job Ndugai eneo la Nane nane kwa Nauli ya Shilingi 3000, pikipiki na bajaji ni Tsh 15,000/-., usafiri unapatikana kuanzia saa 3:30 asubuhi hadi saa 12:30 jioni. Ufikapo hombolo shukia kituo cha Afya na utaiona shule upande wa kulia, umbali wa mita 50. Muhula wa Masomo unaanza tarehe 1 July, 2024 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 30 June, 2024. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 15 July, 2024

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare ya Shule**

i. Sare ya shule ni suruali ya bluu-nyeusi (dark-blue, kitambaa grade one) pea mbili zenye marinda mawili kila upande, mifuko miwili ya pembeni na mmoja wa nyuma, upana wa chini ni 16, suruali fupi na zinazobana chini haziruhusiwa kabisa.
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu, tai ya blue-nyeusi ndefu.
iii. Sare ya Michezo ni trak suti rangi ya kijivu na nyeusi isiyo na maandishi moja, raba nyeupe pea moja, bukta nyeusi, fulana ya njano isiyo na maandishi.
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeusi;
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;Sweta rangi ya bluu nyeusi (dark-blue) lenye V-shape shingoni moja
vii. Nguo za kushindia (*shamba dress*)suruali rangi ya damu ya mzee pea mbili na fulana mbili za njano zisizo na maandishi.
viii. Mwanafunzi aje na tisheti ya kijivu (form six) isiyo na maandishi(Pia inaweza kupatikana kwenye duka la shule).

N.B KWA MWANAFUNZI MWENYE BIMA YA AFYA ANASHAURIWA KUJA NAYO SHULENI KWA AJILI YA KUMSAIDIA KUPATA MATIBABU PINDI AWAPO SHULENI.KWA WASIO NA BIMA YA AFYA MZAZI ANAWEZA KUMPATIA MWANAE FEDHA TSH 5000/= KWA AJILI YA KUMTENGENEZEA BIMA YA AFYA.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapasw kujanayo Shuleni:-**

i. Madaftari 6 'counter book require 4'
ii. **Ream za karatasi (A4)** Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Kikokotoa cha kisayansi (Scientific calculators) yenye uwezo wa angalau **fx 991** kwa wanafunzi wote.
vi. Godoro moja lenye ukubwa wa 2.5 x 6.
vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya blue bahari, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (*cha pembe nne rangi ya blue bahari);*
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
x. Ndoo 1 ndogo (lita kumi) chupa ya plastiki moja ya kuhifadhia maji ya kunywa
xi. Sanduku la bati imara (tranka) lenye makufuri mawili.
xii. Jembe lenye mpini moja na soft broom moja kwa wanafunzi wote.
xiii. Hard broom moja na squezeer moja kwa wanafunzi wa PCM
xiv. Fagio ya chelewa yenye mpini 1 kwaajili ya kufagilia nje,kwanja moja kwa wanafunzi wa PCB.
xv. Nakala ya cheti cha kuzaliwa, hati ya matokeo ya Kidato cha Nne (result Slip)

**ANGALIZO**

Mwanafunzi asije na mizigo au begi kubwa shuleni, aje na Tranka moja tu na begi dogo la kubebea vitabu akiwa shulen na vitu wakati wa likizo. Ni marufuku kuja na nguo za ziada.

### 2.3 Michango mbalimbali

Utatakiwa kulipa michango ifuatayo:-

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Jumla ya michango kwa kila mwanafunzi ni shilingi **80,000.00** (Elfu Themanini tu). Malipo yote yalipwe kupitia Benki ya NMB au Wakala yeyote nchini kwa kupitia akaunti namba **50501200074** yenye jina la **Hombolo sekondary** Stakabadhi zote za malipo (bank pay-in-slip) ziletwe Shuleni zikiwa na jina la mwanafunzi, kidato na tahasusi yake nyuma.

**ANGALIZO**: Shule haitahusika na malipo yoyote yatakayofanywa nje ya mfumo wa benk.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);

iv. Kuwahi katika shughuli zote za shule utakazopewa, hususani utunzaji wa bustani ya mboga na usafi.

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kufuga nywele, wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;

xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3.3 Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

4. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

**KARIBU SANA HOMBOLO SEKONDARI**

**Joseph C. Kavalambi**
**Mkuu wa Shule**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI HOMBOLO
S. L. P. 1719
DODOMA

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0688 227150**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0713 042844**
- **Mwandamizi Taaluma 0764 892370**
- **Mwandamizi Malezi Bweni 0683 104790**

## Fomu Na. 1 AHADI YA MZAZI / MLEZI

Mimi_________________________________________waS.L.P____________ Mji_________________Simu(WhatsApp) ________________na mwenye picha hapo juu. Ambaye kazi yangu ni ______________natamka hapa kama mzazi /mlezi wa ___________________. Ninakubali kwa hiari yangu mwanangu asome katika

Shule ya Sekondari ________________ kuanzia tarehe ________________. Ninaahidi kama ifuatavyo:-

1. Kwamba nimekubali chaguo alilopewa mwanangu na sitamruhusu kubadilisha hadi apate kibali cha maandishi kutoka kwa mamlaka husika.
2. Ninaahidi kumpatia mwanangu vifaa vyote kama vilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga ikiwemo SARE KAMILI ya shule bila kuharibu chochote.
3. Ninatambua ya kuwa walimu wanahitaji ushirikiano wangu katika kumpatia mwanangu elimu na nitashirikiana nao bega kwa bega kwa masuala yanayomuhusu mwanangu kitaaluma na nidhamu ili aweze kufikia malengo yake na ya Taifa.
4. Naahidi kuwa endapo mwanangu ataenda kinyume na taratibu zilizoainishwa katika fomu hii achukuliwe hatua stahili za kinidhamu kama alivyoorodheshewa.

Jina:________________________ saini_______________

Tarehe:____________Uhusiano na mwanafunzi:____________

Fomu NA.2

AHADI YA MWANAFUNZI

| picha |
|---|

Mimi______________________________Mwanafunzi Wa kidato cha Tano tahasusi______________ mwaka wa masomo______________. Ninakiri kusoma, kuelewa na kuahidi kutii taratibu zote zilizoainishwa katika fomu iliyotumwa kwangu na Mkuu wa shule ya Sekondari Hombolo. Nitatoa ushirikiano wa kutosha kwa walimu wangu na shule kwa ujumla katika muda wangu wote nitakaokuwa shuleni ili niweze kupata elimu na kuendeleza jamii na Taifa langu.

Jina:_______________________________________Saini_______________

Tarehe: ___________________

Fomu Na. 3

KIAPO CHA MZAZI / MLEZI

Mimi:______________________________wa S.L.P_________Mji______________ Simu Na_____________________. Nakiri kukaa na kuzungumza na mwanangu juu ya taratibu na sheria za shule na ninaahidi kumsaidia na kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Mkuu wa Shule na walimu kwa muda wote ambao mwanangu atakapokuwa katika shule hii. Ninatambua madhara ya mwanangu kutembelewa na wageni wasioeleweka wakati akiwa shuleni na ninaomba shule iwatambue watu watatu (3) ambao wanahusika katika muda wote ambao atakuwa shuleni nao ni:-(ambatanisha picha passport size zao)

*Picha ya ndugu wa Kwanza*

Jina:____________________________________________ Kazi_______________________
Makazi:________________________________ Simu: ___________________________
Uhusiano na mwanafunzi:___________________________________________________

*Picha ya ndugu wa Pili*

Jina:____________________________________ Kazi:_____________ _________
Makazi: _________________________________ Simu: ______________________
Uhusiano na mwanafunzi:_____________________________________________

*Picha ya ndugu wa Tatu*

Jina:_____________________________________ Kazi:_____________ ________
Makazi:__________________________________Simu: ____________________
Uhusiano na mwanafunzi:____________________________________________

Saini ya mzazi/ mlezi:_________________________Tarehe:_________________

<u>Fomu Na. 4</u>

UTHIBITISHO WA AFYA

Hombolo Secondary school,
P.O. BOX 1719,
DODOMA.

MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by Medical Officer from a known Public Hospital or Health Centre in respect to all entrants

Full name……………………………………Age………Sex…………year…..

1. Blood count (Red and White) ………………………………………..
2. Urinalysis Test ………………………………………………………..
3. Syphilis test…………………………………………………………..
4. T.B…………………………………………………………………….
5. Eye Test ……………………………………………………………….
6. Ears……………………………………………………………………
7. Spleen…………………………………………………………………
8. Abdomen ……………………………………………………………

ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical impairment, family disease, chronic infections etc.

…………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………

I certify that the above named individual is fit to pursue studies as stated above

| | |
|---|---|
| ……………………………… | …………………………………… |
| Name and Designation | Signature and Official stamp |
| ……………………………… | …………………………… |
| STATION | DATE |

**NOTE:**

1. Medical officer during the course of this Examination please attend the individual according to any diagnosed case.
2. The dully filled form must be handed to the Head of the School during registration week, under No circumstances should a student be registered without certification of his/her physical fitness.